Jumanne Mei 02, 2023.

# NCHI YETU

*Tanzania Imara, Kazi Iendelee.*

www.maelezo.go.tz | Toleo la 623 | Idara ya Habari MAELEZO | TANZANIA



IDARA YA HABARI
Maelezo
MSEMAJI MKUU WA SERIKALI

HALIUZWI


UHURU NA UMOJA



# Wizi wa Mitihani: Tusipoziba Ufa Tutajenga Ukuta

Na Adolf F. Mkenda

Mitihani ya mwisho ya kidato cha sita imeanza rasmi tarehe mbili mwezi huu wa tano. Mitihani hii itakamilika tarehe ishirini na mbili mwezi huu. Mitihani hii itafanyika pia sambamba na mitihani ya wanafunzi wanaosomea ualimu. Kadhalika wapo wanafunzi ambao matokeo yao ya kidato cha nne yalifutwa na wameruhusiwa kurudia mitihani yao katika kipindi hiki cha mitihani.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dokta Samia Suluhu Hassan, kupitia akaunti yake ya Twitter, ametuma salamu za heri kwa watahiniwa wote.

Mimi, pamoja na wenzangu wote kwenye Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tunaungana na Rais wetu kuwatakia watahiniwa wote kila la heri kwenye mitihani hii. Pamoja na salamu hizi, natoa wito kwa watahiniwa wote kuzingatia masharti na taratibu zote za mitihani. Kutokuzingatia masharti ya mitihani kunaweza kupelekea mtahiniwa kufutiwa matokeo yake ya mitihani. Waalimu, wasimamizi wa mitihani, wazazi na walezi wote kwa pamoja tuhimize watahiniwa wetu wafanye mitihani yao kwa kuzingatia masharti na taratibu zilizowekwa.

Napenda kutumia fursa hii pia kutoa wito kwa Watanzania wote tushirikiane kutokomeza udanganyifu na wizi wa mitihani. Ni kweli kwamba tatizo la wizi na udanganyifu wa mitihani ni dogo sana hapa nchini, lakini tusipoziba ufa tutajenga ukuta. Tutakosea sana tukifumbia macho tatizo hili hata kama ni dogo sana. Kufumbia macho na kunyamaza hakuondoi tatizo. Kuficha tatizo na kutokuchukua hatua madhubuti ni sawa na kulea na kukuza tatizo.

Madhara ya kuenea kwa wizi na udanganyifu wa mitihani ni makubwa sana kwa Taifa letu. Kwanza, wizi na udanganyifu wa mitihani unaathiri haki za watahiniwa wanaofanya mitihani yao kwa uadilifu. Kwa kawaida wizi na udanganyifu wa mitihani unaoratibiwa na watumishi wasio waaminifu hunufaisha watahiniwa wenye uwezo zaidi wa kifedha; wenye uwezo mdogo wa kiuchumi hawawezi kulipa gharama za mitihani ya wizi. Pili, wizi na udanganyifu wa mitihani unadumaza weledi katika taifa letu na kukuza ubabaishaji. Hatimae tutakuwa na madaktari wababaishaji, marubani wababaishaji, waalimu wababaishaji na kadhalika. Tatu, wizi na udanganyifu wa mitihani unaharibu malezi ya watoto na vijana wetu kwa kufundisha wizi na udanganyifu kwama njia ya kutafuta mafanikio.

Serikali itaendelea kuchukua hatua kali dhidi ya wote wanaojihusisha na wizi na udanganyifu wa mitihani. Tunao maofisa ambao wako mahabusu wakikabiliwa na mashtaka ya kuratibu na kuwezesha wizi na udanganyifu wa mitihani. Zipo baadhi ya shule ambazo zimefutwa kama vituo vya mitihani kwa sababu ya wizi na udanganyifu wa mitihani. Endapo itatulazimu, tutafuta usajili wa shule zinazoratibu wizi na udanganyifu wa mitihani. Ni matumaini yetu kwamba hatutalazimika kufuta usajili wa shule, lakini ni vyema ikafahamika kuwa hii ni hatua inayoweza kuchukuliwa.

Endapo sote tutashikamana na kukemea udanganyifu kwenye mitihani hapana shaka tutafanikiwa kutokomeza jambo hili. Ni jukumu la kila mmoja wetu kuwa macho na kutoa taarifa endapo tutaona dalili zozote za udanganyifu kwenye mitihani. Mtu yeyote atakaekuwa na taarifa kuhusu vitendo vya wizi na udanganyifu wa mitihani tunamuomba atoe taarifa kwa mamlaka yeyote ya Serikali iliyo karibu nae. Namba ya simu ifuatayo itatumika pia kupokea taarifa zozote kwa siri za wizi na udanganyifu wa mitihani:

**0759 360 000**

**Taarifa pia inaweza kutumwa kwa baruapepe ifuatayo:**

**esnecta@necta.go.tz**

Mwisho napenda tena kuwatakiwa watahiniwa wote kila la heri katika mitihani yao.






# Wajawazito Kupimwa Vipimo vya Awali Bila Malipo

Na Catherine Sungura - Dodoma.

Waziri wa Afya, Mhe.Ummy Mwalimu ametaka akina mama wajawazito wanaofika kwenye Kliniki za Uzazi, Mama na Mto kupima wingi wa damu, mkojo, kuangalia wingi wa protini, shinikizo la damu pamoja na kusikiliza mapigo ya moyo ya mtoto bila kutozwa gharama zozote.

Haya ameyasema leo wakati wa kukabidhi vifaa tiba vya kuboresha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto kwa vituo ishirini vya halmashauri za Mkoa wa Dodoma vyenye thamani ya shilingi milioni 45 .

Waziri Ummy amesema kuwa vipimo hivyo ni muhimu kwa wajawazito ili kuweza kuepusha kifafa cha mimba na vifo kwa wajawazito.

“Ili kuweza kumuokoa mama mjamzito anapofika kliniki ni vyema kupimwa vipimo hivyo muhimu, vipimo hivi vyote ni bure na ni lazima viwepo kwenye vituo vya kutolea huduma za afya vyote nchini," amesema Mhe. Ummy.
Ameendelea kusema kuwa, Serikali itahakikisha upatikanaji wa 100% wa dawa za kuzuia kutoka damu wakati wa kujifungua, dawa za kuongeza damu na dawa za kuzuia kifafa cha mimba katika vituo vya afya vya umma nchini.

“Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshatimiza wajibu wake kwa kujenga majengo,kuboresha miundombinu, kuongeza ajira pamoja na kununua vifaa tiba , hivi sasa tunapata fedha za dawa kila mwezi shilingi bilioni 20, tutahakikisha hizi dawa tatu zinapatika kwa asilimia 100." Amesema Mhe. Ummy

Hata hivyo Waziri Ummy amezitaka timu za afya za uendeshaji za Halmashauri nchini kufanya usimamizi shirikishi kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ili kuwajengea uwezo watoa huduma za afya, “Huu ndio muelekeo wa wizara, twende kwenye masuala ya kuwawezesha wataalamu wetu kwenye vituo vya afya na kuona kipi kinafanyika tunaweza kupunguza vifo vya akina mama wajawazito na watoto wachanga kama tutaongeza kutoa huduma bora za afya," amesisitiza.

Akitaja taarifa za Utafiti wa Idadi ya Watu na Afya na Utafiti wa Kiashiria cha Malaria (DHS/MIS) ya mwaka 2022 zinaonesha kuwa nchi imepiga hatua katika viashiria vingi vya afya vya mama na mtoto mathalani vifo vya watoto chini ya miaka mitano vimeshuka kutoka 67 kati ya vizazi hai 1000 mwaka 2015/2016 hadi 43 kwa kila vizazi hai 100.

“Mahudhurio kliniki ya wajawazito mara nne na zaidi kutoka 53% hadi 65%, aidha, wajawazito wanaojifungulia katika vituo vya huduma wameongezeka kutoka 63% hadi 81% na wanaojifungua chini ya uangalizi wa mtoa huduma mwenye ujuzi kutoka 66% hadi 85%," amefafanua Waziri Ummy.



# Serikali Kuingia Mkataba na Watoa Huduma za Mawasiliano Kufikisha Huduma katika Maeneo 763

Na Jacquiline Mrisho - MAELEZO

Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Mhandisi Kundo Mathew amesema kuwa mwezi huu wa Mei, 2023, Serikali inatarajia kuingia mkataba na watoa huduma ili kuweza kufikisha huduma za mawasiliano katika maeneo 763 nchini.

"Ili kuendelea kuongeza wigo wa huduma za mawasiliano nchini, Serikali pia, imeshaanza kufanya tathmini katika vijiji 2,116 na tathmini itakapokamilika, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kufikisha huduma za mawasiliano katika vijiji hivyo", aliongeza Mhe. Kundo.

Ameyasema hayo wakati akijibu maswali bungeni ambapo swali la msingi liliulizwa na Mbunge wa Viti Maalum, Mhe. Zuena Bushiri lililohoji je, ni lini umeme utafungwa kwenye mnara wa halotel uliopo kata ya Ngujini wilayani Mwanga?.

Ambapo Naibu Waziri Kundo alijibu kuwa jukumu la kuunganisha umeme kwenye minara ya mawasiliano ya simu nchini, ikiwemo ile iliyojengwa kwa ruzuku ya Serikali, ni la watoa huduma ambapo ni pamoja na gharama za kuunganisha umeme na kuendesha minara husika.

Mhe. Kundo ameongeza kuwa, Serikali itaendelea kusimamia huduma za mawasiliano nchini kwa kuhakikisha huduma zinazotolewa zinakidhi matakwa ya leseni zinazotolewa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

Aidha, amesisitiza kuwa Serikali haiwezi kupuuza malalamiko ya wananchi, hivyo ametoa maelekezo kwa TCRA kufanyia kazi malalamiko ya wananchi ili kuhakikisha changamoto za wananchi zinatatuliwa.



# Sheria ya Habari 2016 Inawataka Waajiri Kuwakatia Waandishi wa Habari Bima ya Maisha

Na Lilian Lundo - MAELEZO

Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Habari - MAELEZO, Zamaradi Kawawa amesema Sheria ya Habari ya Mwaka 2016 inawataka waajiri kuwakatia Waandishi wa Habari Bima ya Maisha kutokana na changamoto wanazozipa katika kazi zao za kila siku.

Zamaradi ameyasema hayo leo Mei 2, 2023 Zanzibar wakati wa majadiliano ya Mada ya Usalama wa Waandishi wa Habari katika maadhimisho ya Uhuru wa Vyombo vya habari ambayo kilele chake ni Mei 3, 2023.

"Sheria ya Huduma za Habari ya Mwaka 2016 inapigiwa sana kelele lakini ina mambo mengi muhimu, kama vile katika kifungu cha 58 sheria inawataka waajiri kuwakatia Bima ya Maisha Waandishi wa Habari, kutokana na madhila wanayokutana nayo katika kazi zao za kila siku," amesema Zamaradi.

Ameendelea kusema kuwa, Uandishi wa Habari ni moja kati ya kazi ambayo inahatarisha maisha kutokana na kutakiwa kuandika habari hata katika matukio ya hatari kama vile vita au magonjwa ya mlipuko kama Corona.

"Kutokana na hatari wanazokutana nazo Waandishi wa Habari pindi wanapotimiza wajibu wao, serikali imeona kuna umuhimu wa Waandishi wa Habari kukatiwa Bima ya Maisha, hivyo Sheria ya Huduma za Habari ya Mwaka 2016 itakapoanza kufanya kazi itawasaidia Waandishi wa Habari kupata haki ya kuwa na Bima ya Maisha ambayo itawasaidia pindi watakapokumbana na jambo lolote la hatari katika kazi zao," amesema Zamaradi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC), Keneth Simbaya amewataka Waandishi wa Habari kutumia mjadala huo kujadili masuala yote ya usalama wa Waandishi kwa Habari ikiwemo kutolipwa mishahara.

"Tujue kwanza chanzo cha madhali tunayopitia Waandishi wa Habari, tusipofanya hivyo tutajikuta tunaongelea madhali ya upande mmoja. Kutolipwa mishara, kutokuwa na taaluma ya kazi unayofanya, hizo pia ni madhali ambayo yanahusiana na usalama wa Mwandishi wa Habari," amesema Simbaya.



# Wanawake Tushirikiane Kuendeleza Mapambano - Shebe

Na Mwandishi Wetu- MAELEZO

Mwenyekiti wa Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), Bi. Joyce Shebe ametoa wito kwa Wanawake kubeba agenda ya Wanawake tunapoelekea katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu unaotarajia kufanyika mwaka 2025.

Bi. Joyce ameyasema hayo leo Zanzibar wakati wa kujadili mada kuhusu Jinsia na Uongozi kwa Wanawake wakati wa Kongamano la wadau wa Habari kuelekea maadhimisho ya miaka 30 ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari yanayofanyika Zanzibar.

"Katika Chaguzi zetu zijazo tubebe agenda za wanawake kwa lengo la kuwasaidia wenzetu watakaojitokeza, tunapeana moyo na tushirikiane," amefafanua Bi. Joyce.

Aidha, amebainisha kuwa harakati hizo zilianza muda mrefu na matokeo ni mengi, na safari bado ni ndefu hivyo yapaswa wanawake kushirikiana kuendeleaza mapambano

Mbali na hayo Bi. Joyce ametoa wito kwa Wanahabari kujituma ili kuweza kutimiza ndoto na maono waliyonayo.

Leo Mei 2, 2023 ni siku ya pili ya kuelekea kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari, ambapo kilele chake ni tarehe 3 Mei, 2023. Maadhimisho hayo yamebebwa na Kaulimbiu inayosema "Kuunda Mustakabali wa Haki, Uhuru wa Kujieleza kama Kichocheo cha Haki Nyingine Zote za Kibinadamu".




# Ubora Habari za Mitandaoni Wakosolewa

Na Waandishi Wetu

Wanahabari na wazee wamekosoa ubora wa baadhi ya habari zinazotolewa mitandaoni wakisema zina madhara kwa jamii kutokana na kutofuata misingi ya taaluma ya uandishi wa habari.

Akizungumza na waandishi wa habari hii leo jijini Zanzibar, Mwanahabari na Mvumbuzi wa Taasisi ya Digital Safaris, Bi. Tanjana Francis amesema habari lazima iwe na malengo mema.

"Ushauri wangu kwa vyombo husika ni kwamba waangalie namna ya kudhibiti upashanaji wa habari, hapo tutakuwa tumeendelea katika taaluma hii, lakini pia waangalie madhara yanayopatikana baada ya habari kutolewa.

"Wazuie kutoa habari yenye madhara, na pale inapotokea wamechapisha mitandaoni habari hizo basi wazitoe mara moja ili kuzuia ukubwa wa madhara," ameeleza Bi. Tanjana.

Naye, Mwanahabari Mkongwe, Bw. Ali Saleh ametoa wito kwa wanahabari wa mitandaoni kukosoa kwa busara.

Kwa upande wake, Mkazi wa Fuoni - Zanzibar, Mzee Ali Hamad Ntwana amesema waandishi wa habari za mitandaoni wanafanya kazi kubwa ya kuelimisha jamii kwa wakati japokuwa haraka ya kupasha habari huwafanya watoe taarifa isiyohakikiwa vyema.

Naye, Bi. Mwahija Kombo Mtumweni ameeleza kwamba habari nyingi za mitandaoni zinahusu udaku wa wasanii unaohusiana na matukio ya faragha ambayo huenda yakaharibu maadili ya Kitanzania na Kizanzibari.



# Washauriwa Kuheshimu Haki za Watoto Katika Taarifa Wanazozitoa

Na Waandishi Wetu

Wanahabari na wazee wamekosoa ubora wa baadhi ya habari zinazotolewa mitandaoni wakisema zina madhara kwa jamii kutokana na kutofuata misingi ya taaluma ya uandishi wa habari.

Akizungumza na waandishi wa habari hii leo jijini Zanzibar, Mwanahabari  na Mvumbuzi wa Taasisi ya Digital Safaris, Bi. Tanjana Francis amesema habari lazima iwe na malengo mema.

"Ushauri wangu kwa vyombo husika ni kwamba waangalie namna ya kudhibiti upashanaji wa habari, hapo tutakuwa tumeendelea katika taaluma hii, lakini pia waangalie madhara yanayopatikana baada ya habari kutolewa.


"Wazuie kutoa habari yenye madhara, na pale inapotokea wamechapisha mitandaoni habari hizo basi wazitoe mara moja ili kuzuia ukubwa wa madhara," ameeleza Bi. Tanjana.

Naye, Mwanahabari Mkongwe, Bw. Ali Saleh ametoa wito kwa wanahabari wa mitandaoni kukosoa kwa busara.

Kwa upande wake, Mkazi wa Fuoni - Zanzibar, Mzee Ali Hamad Ntwana amesema waandishi wa habari za mitandaoni wanafanya kazi kubwa ya kuelimisha jamii kwa wakati japokuwa haraka ya kupasha habari huwafanya watoe taarifa isiyohakikiwa vyema.

Naye, Bi. Mwahija Kombo Mtumweni ameeleza kwamba habari nyingi za mitandaoni zinahusu udaku wa wasanii unaohusiana na matukio ya faragha ambayo huenda yakaharibu maadili ya Kitanzania na Kizanzibari.

# Clubhouse




**@Maelezo News (People)**
**@Msemaji Mkuu wa Serikali (Clubs)**

Ofisi ya Msemaji Mkuu wa Serikali.
Idara ya Habari MAELEZO

Imeandaliwa na Ofisi ya Msemaji Mkuu wa Serikali | IDARA YA HABARI MAELEZO